

Majuto ni mjukuu. Angalia kisa cha huyu dada

By SW - Melkisedeck Shine · December 22, 2016

Hadithi za Kiswahili: Historia, Mapenzi na Maisha · #Hadithi za Kufundisha

Dada mmoja aliyejulikana kwa jina la Angel, alikuwa anafanya biashara ya kujiuza ili aweze kuweka kitu tumboni mwake. dada huyo alikuwa na wateja wamaana na mapedeshee wengi sana kwa hiyo kwa siku yeye kuondoka na laki 4 au 5 ilikuwa ni kawaida sana.

Siku moja dada Angel aliamua aende hospitali ili akatoe mimba aliyokuwa nayo tumboni mwake, alifanikiwa na kutoa mimba ile lakini baada ya kumaliza utoaji wa miamba alimuomba daktari atoe kizazi kabisa ili asipate tabu ya kuja kutoa mimba kila mara!

Daktari alifanya kama alivyoambiwa. Dada Angel alirudi mtaani na kuendelea na biashara ya kujiuza.

Siku moja ilikuwa jumapili Angel alikutana na rafiki yake wa muda mrefu waliyokuwa wanaishi wote enzi za utoto wao, rafiki yake huyo alimwambia Angel waende kanisani, ili kuficha aibu ya biashara aliyokuwa anafanya; dada Angel alikubari na wakaamua kwenda wote kanisani.

Siku hiyo Angel alilielewa sana neno la Mungu kutoka kwa mchungaji na akaahidi kuwa jumapili ijayo ataenda, basi ikawa tabia mpya ya dada Angel akawa kila siku anafanya biashara zake za kujiuza na jumapili anaenda kanisani..

Kadri siku zinavyozidi kwenda dada Angel akaanza kupunguza biashara ya kujiuza na kumgeukia Muumba mpaka akaacha kabisa tabia ya kujiuza na kuanza kufanya shughuli nyingine zilizokuwa zinamuingizia kipato.

Siku moja Angel alienda kanisani na alipokuwa ameketi mchungaji alimfuata na kumwambia "nimeoteshwa kuwa ww ndiyo utakuwa mke wangu wa kufa na kuzikana" dada Angel alishtuka na alimtazama mchungaji na kumwambia "mchungaji umekurupuka mimi kamwe siwezi kuwa mke wa mtu na kamwe siwezi kuzaa" alimaliza Angel na kuondoka kanisani.

Kila wiki aliyokuwa anaenda kanisani dada Angel alikutana na maneno yale yale kwa mchungaji na mchungaji alimwambia "nimeota umepata ujauzito na umenizalia watoto wanne" Angel alimuangalia mchungaji na kusimama na msimamo wake ulele ule.

Siku zilizidi kwenda lakini kutokana na mchungaji kuendelea kusema maneno yale yale basi ilibidi dada Angel akubali na akakubali kuolewa na mchungaji na wakafunga ndoa na ndoa yao ilikuwa ya furaha sana.

Kadri siku zilivyozidi kwenda dada angel alianza kuona mabadiliko mwilini mwake na kuamua kwenda katika ile hospitali aliyowahi kwenda mwanzo kutoa mimba na kumkuta daktari aliyemfanyanyia utoaji wa mimba siku za nyuma, baada ya daktari kumona Angel akajua amekuja kwa shida nyingine ikabidi amuulize "Dada Angel nikusaidie nini tena dada yangu" Angel alijibu kuwa anahisi anadalili za ujauzito, Daktari alicheka sana baada ya kuambiwa hayo majibu kutoka kwa angel na daktari alimwambia "Dada Angel naona umechanganyikiwa enh dada yangu?? mimi ndiye nilitoa kizazi chako leo iweje uwe na mimba acha kuchekesha walionuna"

Angel alimwambia daktari chukua vipimo kapime, kweli daktari alifanya hivyo na baadae

akarudi mikono inamtetemeka na kumwambia angel "Dada angel nipeleke na mimi kwa huyo uneyebuabudu nami niweze kumuabudu maana ni mkweli na anasaidia wanyonge,

Ndugu yangu hata kama upo katika wakati mgumu kiasi gani lakini kumbuka yupo anaweza kufanya ugumu wa mambo yako kuwa mepesi kama unatafuna karanga. hakuna kinachoshindikana kwa Mungu,comment AMINA kama unaamini hakuna kinachoshindika na kwa jina lake yeye muumba na kama unaamini magumu yako yote yenaweza kuwa mepesi kupindukia

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=731>